# Ajali ya mabasi yaua 6, kujeruhi 4 Mkuranga, madereva wakimbia

Na Mwandishi Wetu

WATU sita wamepoteza maisha na wengine wanne kujeruhiwa kufuatia ajali ya barabarani iliyohusisha basi la Kampuni ya Mahuta Express na basi dogo la abiria aina ya Toyota Coaster katika eneo la Kimanzichana wilayani Mkuranga mkoani Pwani.

Ajali hiyo ilitokea jana saa 11:00 alfajiri katika Barabara Kuu ya Dar es Salaam kuelekea Lindi ndani ya Mkoa wa Kipolisi Rufiji.

Kwa mujibu wa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kipolisi Rufiji, Protas Mutayoba ajali hiyo ilihusisha basi la Mahuta Express lenye namba za usajili T224 DCN aina ya Yutong lililokuwa likitoka Newala kwenda Dar es Salaam na basi dogo la abiria aina ya Toyota Coaster lenye namba za usajili T308 DZE lililokuwa likitoka Dar es Salaam kuelekea Somanga.

Kamanda Mutayoba alisema baada ya ajali hiyo kutokea, madereva wa vyombo hivyo viwili walikimbia na kutoweka, huku juhudi za kuwatafuta zikiendelea kwa kushirikiana na wamiliki wa magari hayo.

Alisema watu sita waliopoteza maisha katika ajali hiyo ni wanaume watano na mwanamke mmoja. Miili ya marehemu imehifadhiwa katika chumba cha kuhifadhia maiti cha Hospitali ya Wilaya ya Mkuranga kwa ajili ya taratibu nyingine.

Aidha, watu wanne walijeruhiwa katika ajali hiyo, wakiwemo wanawake wawili na wanaume wawili. Majeruhi hao walikimbizwa Hospitali ya Kilimahewa kwa matibabu.

Jeshi la Polisi Mkoa wa Kipolisi Rufiji limeendelea na uchunguzi wa chanzo cha ajali hiyo, huku likitoa wito kwa madereva na watumiaji wote wa vyombo vya moto kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za usalama barabarani ili kuepusha ajali zinazoweza kusababisha vifo, majeruhi na hasara za mali. Kamanda Mutayoba alisema ushirikiano wa wananchi katika kutoa taarifa sahihi utasaidia kufanikisha uchunguzi wa tukio hilo na kuwabaini wahusika.

CamScanner